# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**TAARIFA KWA UMMA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO, VYUO VYA UALIMU NA VYUO VYA ELIMU YA UFUNDI MEI, 2022

**MEI,2022**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO, VYUO VYA UALIMU NA VYUO VYA ELIMU YA UFUNDI MEI, 2022

**Ndugu Wananchi;**

Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, sayansi na Teknlolojia na Baraza la Mitihani la Tanzania imekamilisha Zoezi la Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Elimu ya Ufundi vya Serikali Mwaka 2022. Zoezi hili limefanyika kwa kuzingatia takwimu za matokeo ya Wanafunzi waliofanya Mtihani wa Kidato cha Nne Mwaka 2021, kutoka Tanzania Bara.

**Ndugu Wananchi;**

Watahiniwa katika mtihani wa kidato cha Nne kwa mwaka 2021 waliopata Daraja la I – III walikuwa **173, 422** wakiwemo wasichana **75,056** na wavulana **98,366.** Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi wenye sifa ya kujiunga na kidato cha Tano, vyuo vya Ualimu na vyuo vya Ufundi ni **167,515** wakiwemo wasichana **71,433**. Idadi hiyo ya wanafunzi wenye sifa imejumuisha wanafunzi wenye Mahitaji Maalum **508** wakiwemo wasichana **217** na wavulana **291**. Hii ni ongezeko la wanafunzi **19,388** kwa kulinganisha na wanafunzi **148,127** waliokuwa na sifa kwa mwaka **2021.**

**Ndugu Wananchi;**

Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Elimu ya Ufundi mwaka 2022**,** ni kutoka Shule za Serikali, zisizo

za Serikali, watahiniwa wa kujitegemea waliofanya mtihani kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima waliokidhi vigezo na waliosoma Nje ya nchi ambao matokeo yao yamefanyiwa ulinganifu wa Baraza la Mtihani Tanzania (NECTA).

**Ndugu wananchi,**

Wanafunzi **153,219** wakiwemo wasichana **67,541** na wavulana **85,678** sawa na asilimia **91.8** ya wenye sifa, wamechaguliwa kujiunga na Shule za sekondari Kidato cha Tano, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Elimu ya Ufundi mwaka, 2022 katika mchanganuo ufuatao;

- Wanafunzi **90,825** wakiwemo wasichana **43,104** wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari **499** za Serikali zikiwemo Shule mpya **22** za Serikali zilizoanza mwaka, 2022. Kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha Tano, wapo wanafunzi wenye Mahitaji Maalum **481** ambao kati yao wasichana ni **204**. Kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, wanafunzi **41,401** wakiwemo wasichana **17,390** watajiunga kusoma tahasusi za Sayansi na Hisabati na wanafunzi **49,133** wakiwemo wasichana **25,508** watajiunga kusoma tahasusi za masomo ya Sanaa, Lugha na Biashara;

- Wanafunzi **1,880** wakiwemo wasichana **757** wamechaguliwa kujiunga na fani mbalimbali katika Vyuo **03** vya Elimu ya Ufundi ambavyo ni Chuo cha Ufundi cha Arusha (**ATC**), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (**DIT**) na Chuo cha Usimamizi na Maendeleo ya Maji (WDMI);

- Wanafunzi **2,294** wakiwemo wasichana **1,127** wamechaguliwa kujiunga na Vyuo vya Afya ngazi ya Stashahada;

- Wanafunzi **2,674** wakiwemo wasichana **1,366** wamechaguliwa kujiunga na Vyuo vya Ualimu ngazi ya Stashahada ya Sayansi, Hesabu na TEHAMA;

- Wanafunzi **6,457** wakiwemo wasichana **3,168** wamechaguliwa kujiunga na Astashahada ya Elimu Maalum, Awali, Michezo, Msingi na Ualimu wa Shule zinazofundisha kwa kutumia Lugha ya Kiingereza (English Medium); na

- Wanafunzi **49,089** wakiwemo wasichana **18,019** wamechaguliwa kujiunga na kozi mbalimbali za Astashahada na Stashahada (Certificate and Ordinary Diploma) katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET)

**Ndugu wananchi;**

Kwa kuangalia takwimu za mwaka 2022, kumekuwa na ongezeko la wasichana **7,555** waliochaguliwa kujiunga na kidato cha Tano na vyuo vya ufundi ukilinganisha na mwaka 2021 hata hivyo idadi hii bado ni ndogo kulinganisha na wavulana. Ili kukabiliana na changamoto hii, wizara inaendelea kuboresha miundombinu ya shule ili kuhakikisha wasichana wengi zaidi wanajiunga na kidato cha Tano. Aidha, tunachukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha ujenzi wa shule za wasichana kumi (10) za mikoa

ambapo kila shule itachukua wanafunzi wapatao mia tatu (300) kuanzia mwaka 2023.

**Ndugu Wananchi;**

Pamoja na kuwepo kwa ongezeko la wanafunzi waliojiunga na Kidato cha Tano, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Elimu ya Ufundi kwa mwaka 2022, Jumla ya wanafunzi **14,254** wakiwemo wasichana **3,901** na wavulana **10,353** wamekosa nafasi. Kati yao, wanafunzi **12,876** wana sifa ya kujiunga na kidato cha Tano. Hali hii imetokana na ongezeko kubwa la wanafunzi waliofaulu na waliokuwa na sifa ya kujiunga na Kidato cha Tano na vyuo vya ufundi pamoja na ufinyu wa nafasi za Kidato cha Tano na Vyuo vya Elimu ya Ufundi (NACTVET). Wanafunzi hao wanatarajiwa kujiunga na kidato cha Tano katika awamu ya pili baada ya ukamilishaji wa baadhi ya miundombinu ya shule na vyuo.

**Ndugu Wazazi/walezi**

Muhula wa kwanza kwa wanafunzi wa Kidato cha Tano utaanza tarehe **13 Juni, 2022.** Hivyo, wanafunzi wote waliopangwa kujiunga na Kidato cha Tano kwa mwaka 2022 wanapaswa kuanza kuripoti katika Shule walizopangwa kuanzia tarehe 13 Juni, 2022. Siku ya mwisho ya kuripoti itakuwa tarehe **30 Juni, 2022.** Endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyekosa nafasi. Na kwa kuzingatia kuwa Uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Elimu ya Ufundi umefanyika kwa kuzingatia ufaulu na nafasi zilizopo katika shule; **hakutakuwa na fursa ya kufanya mabadiliko yoyote ya shule kutokana na ukosefu wa nafasi kwenye shule husika.**

Fomu za maelezo ya mahitaji ya kujiunga na Kidato cha Tano *(Joining Instructions)* kwa shule zote za Kidato cha Tano zinapatikana kwenye tovuti ya OR-TAMISEMI kupitia kiunganishi cha www.tamisemi.go.tz na kwa wale waliopangwa kwenye Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi watapokea maelekezo ya namna ya kujiunga kutoka katika Vyuo walivyopangwa. Aidha, Orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Elimu ya Ufundi mwaka, 2022 inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI ya www.tamisemi.go.tz na Baraza la Taifa la Elimu ya Mafunzo ya Ufundi ya www.nacte.go.tz**.**

**Ndugu Wananchi;**

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza walimu, wazazi na walezi wote kwa juhudi walizozifanya katika ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufaulu vizuri. Naomba wazazi/walezi wote tuendelee na moyo huu wa kusimamia na kufuatilia maendeleo ya watoto wetu.

Aidha, nawapongeza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Elimu ya Ufundi. Napenda kuchukua fursa hii, kuwahimiza kuendelea kufanya bidii katika kujifunza ili waweze kufanikiwa kujiunga na mafunzo ya elimu ya juu baada ya kuhitimu Kidato cha Sita na Vyuo vya Elimu na ya Ufundi.

Ninawashukuru Viongozi na Watendaji wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Wananchi kwa ujumla kwa kushiriki kikamilifu katika kuimarisha miundombinu ya shule ikiwemo mabweni na majengo mengineyo yaliyowezesha baadhi ya shule kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano kwa mara ya kwanza mwaka 2022.

**Ndugu Wananchi;**

Nitumie pia fursa hii kutoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kuwa na Shule za Sekondari za Kidato cha Tano katika kila halmashauri inatekelezwa ili kuwezesha wanafunzi wote wanaofaulu Mtihani wa Kidato cha Nne kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya Kidato cha Tano na Sita. Mikoa ihakikishe inakuwa na tahasusi zote za msingi katika shule zinazoanzishwa ili kuwapunguzia wazazi/walezi gharama za usafiri kwenda shule za mbali. Aidha, kutokana na ongezeko la ufaulu wa masomo ya Sayansi, ninaelekeza shule zitakazoanzishwa za Kidato cha Tano ni **lazima ziwe na Tahasusi za Sayansi. Pia, shule ambazo zina tahasusi za sanaa pekee ziongeze tahasusi za sayansi.**

**Ndugu Wananchi;**

Pamoja na maelekezo haya, kwa mwanafunzi, mzazi/mlezi atakayekuwa na suala linalohitaji maelekezo au ufafanuzi zaidi aende katika Ofisi za Elimu za Mikoa na Halmashauri au apige simu kwenye namba ya Kituo cha Huduma kwa wateja cha OR-TAMISEMI kwa **namba za simu 026 2160210 au 0735 160210.**

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Mhe. Innocent Bashingwa (**MB**)

**WAZIRI WA NCHI, OR-TAMISEMI.**